TANGAZO LA SERIKALI NA. 601 la tarehe 19/7/2023

SHERIA YA PETROLI,

(SURA YA 392)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128(3))*

NOTISI YA KIBALI CHA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAMBAZAJI WA GESI ASILIA KWA PAN-AFRICAN ENERGY (T) LIMITED YA MWAKA 2024

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kibali cha Ujenzi wa Miundombinu ya Usambazaji wa Gesi Asilia kwa Pan-African Energy (T) Limited ya mwaka 2024.

Kuanza kutumika

2. Notisi hii itaanza kutumika kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Tafsiri

3. Isipokuwa kama mukhtadha utahitaji vinginevyo-

"mwombaji" maana yake ni kampuni ya Pan-African Energy (T) Limited ya S.L.P. 80139 Dar es Salaam;

Sura ya 414

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji; na

Sura ya 392

"kibali cha ujenzi" maana yake ni kibali kilichotolewa na Mamlaka chini ya kifungu cha 128(1) cha Sheria ya Petroli.

Kutolewa kwa kibali cha ujenzi

4. Mwombaji anapewa Kibali cha Ujenzi cha kujenga bomba lenye urefu wa mita 70 na kipenyo cha milimita 63 na mindombinu inayohusika kwa ajili ya kupeleka gesi asilia kwenye kituo kikuu na kituo cha kujaza gesi asilia cha Tembo Energies CNG kilicho ndani ya kituo cha mafuta cha Mount Meru eneo la Tabata Mwananchi, mkabala na kiwanda cha nguo cha Nida, barabara ya Nelson Mandela, manispaa ya Ubungo, mkoa wa Dar es Salaam kwa kuzingatia vigezo na masharti yafuatayo:

(a) kuzingatia michoro iliyopitishwa, viwango vya kiufundi, ujenzi, uchomeleaji, upimaji na uidhinishaji na njia iliyowekwa alama au sheria

zingine zinazotumika;

(b) kuhakikisha kwamba kituo au miundombinu mingine inayohusika inajengwa kwa kuzingatia viwango vyote vilivyowekwa na kutolewa na Shirika la Viwango la Taifa au sheria zingine zinazohusika;

(c) kuhakikisha kwamba ukaguzi wa mahitaji ya ujenzi wa bomba au miundombinu mingine inayohusika inakidhi uzingatiaji wa vifaa, ujenzi, uchomeleaji, maunganisho na majaribio ya viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango la Taifa;

(d) kuhakikisha kwamba bomba la gesi asilia au miundombinu mingine inayohusika inajengwa kwa kufuata njia iliyoidhinishwa ambayo ilichaguliwa kwa madhumuni ya kupunguza uwezekano wa hatari za mbeleni zitakazosababishwa na maendeleo ya viwanda au miji, kupanuliwa kwa njia na kutoharibu mazingira au sehemu za kihistoria;

(e) kuhakikisha kwamba-

(i) hakuna au kupunguza usumbufu kwa wakazi walio karibu na eneo la ujenzi na

kwamba usalama kwa umma unapewa kipaumbele;

(ii) iwapo ulipuzi utafanyika, unafanywa kwa kuzingatia kanuni, unafanywa na mtu mwenye sifa za kazi ya ulipuzi na kwa kuzingatia usalama kwa umma, mifugo, wanyama, majengo, miundombinu ya simu, umeme, chini ya ardhi na mali nyingine yoyote iliyo karibu na eneo la ulipuzi;

(f) kuhakikisha kwamba-

(i) katika kuandaa njia ya bomba, kila juhudi ya kupunguza uharibifu katika ardhi na kuzuia mazingira yasiyo ya kawaida ya kuziba kwa mifereji ya kupitisha maji na mmomonyoko wa udongo zinafanywa;

(ii) ardhi inarudishwa katika hali iliyokuwepo kwa kadri inavyowezekana;

(g) kuhakikisha kwamba-

(i) katika ujenzi wa bomba linalopita kuvuka reli, barabara, vijito, mito na maziwa, alama za usalama kama vile alama, taa vizuizi vya reli n.k., vitawekwa kwa ajili

ya faida ya usalama wa umma;

(ii) kupita kwa bomba kuvuka vitu hivi kutazingatia kanuni na taratibu zilizopo na makatazo ya mamlaka dhibiti kwenye eneo hili;

(iii) kabla ya ujenzi wa bomba linalopita kuvuka katika maeneo tajwa, taratibu zinawekwa kwa kushirikiana na mamlaka husika ya maeneo au miundombinu linakopita bomba;

(h) kuhakikisha kwamba njia ya bomba imefanyiwa upimaji na kuainishwa na kuwekewa alama ambazo zitaendelea kuwepo wakati wote wa ujenzi kwa mujibu wa masharti yaliyo kwenye kibali kilichotolewa na mmiliki wa njia;

(i) kuhakikisha kwamba bomba linafuata njia kwa kuheshimu upimaji wa njia na alama au kwa kupima wakati wa ujenzi;

(j) kuhakikisha kwamba-

(i) urefu wa mfereji wa bomba ni sahihi kwa kuzingatia eneo la njia, matumizi ya uso wa ardhi, hali ya ardhi na uzito utokanao na barabara na reli;

(ii) upana wa mfereji unaruhusu kuwekwa kwa bomba katika mfereji bila kuharibu rangi yake na kuwezesha kazi ya ufungaji wa bomba kufanyika ndani ya mfereji;

(k) kuhakikisha kwamba hatua zote stahiki ili kulinda kila bomba au vifaa vingine vinavyohusika dhidi ya mafuriko, udongo dhaifu, tetemeko la ardhi au hatari zingine zinazoweza kusababisha bomba kuhama au kupata uzito wa ziada, zinafuatwa;

(l) kuhakikisha kwamba-

(i) bomba linalazwa umbali wa nchi 12 (milimita 300) kutoka kwenye miundombinu mingine iliyo chini ya ardhi ambayo haihusiani na bomba la gesi;

(ii) iwapo haitawezekana kupata umbali huu, bomba lilindwe dhidi ya uharibifu unaoweza kujitokeza kwa kuwa karibu na miundombinu mingine;

(iii) kila bomba liwekwe kwa umbali wa kutosha kutoka kwenye miundombinu chini ya ardhi mingine yoyote ili kuwezesha

bomba kufanyiwa matengenezo na kulilinda dhidi ya uharibifu unaoweza kujitokeza kwa kuwa karibu na miundombinu mingine;

(m) kuhakikisha kwamba vifaa vya kuchomelea ni vya ukubwa na aina sahihi kwa kazi hiyo, na vinawekwa katika hali inayohakikisha uchomeleaji mzuri, kuendelea kwa kazi na usalama wa watu;

(n) kuzingatia-

(i) viwango vya mazingira, afya na usalama vilivyoainishwa na sheria zinazotumika;

(ii) afya na usalama wa watu na vifaa na matumizi ya vifaa vya usalama (PPE) wakati wote kama vile kofia ngumu, miwani na viatu vya usalama na matumizi ya kizima moto vinazingatiwa; na

(o) kuhakikisha kwamba miundombinu yote iliyopo, iwe inasimamiwa na Mamlaka au la, inalindwa dhidi ya uharibifu na kuwaarifu waendeshaji wa miundombinu hiyo kwa kuwaomba wawepo eneo la ujenzi wakati wa

kujenga;

(p) kuhakikisha kwamba eneo la ujenzi limezungushiwa utepe wa tahadhari;

(q) kuweka mifumo ya ulinzi na ufuatiliaji wa bomba ikiwemo mifumo ya kuzuia kutu, valvu za kuondoa mgandamizo, valvu za kujifunga, kipimo cha mgandamizo, mfumo wa kugundua uvujaji wa gesi, mfumo wa kusafisha na kufuatilia unene wa bomba na mifumo ya mawasiliano;

(r) kuhakikisha alama mbalimbali kama vile za kuanisha njia, bomba na alama za uingizaji hewa zimewekwa eneo lote la njia ya bomba; na

(s) kuhakikisha kwamba alama zilizowekwa zinakuwa na alama za onyo zinazofaa, notisi ya tahadhari na namba za simu za dharula. Herufi kwenye notisi ya tahadhari zitaandikwa kwa rangi nyeusi kwa maneno "Onyo au Tahadhari" kwenye ubao wenye rangi nyekundu.

Ukomo wa kibali

5. Kibali kitakoma endapo mwenye kibali atashindwa kuanza ujenzi ndani ya miezi ishirini na nne tangu tarehe ya kutolewa.

Dodoma,
10 Julai, 2024

JAMES A. MWAINYEKULE
*Mkurugenzi Mkuu*